

# Uanafunzi na mafunzo kazini

## Taarifa kwa wazazi na walezi

---

Uanafunzi na mafunzo kazini ni njia za kujifunzia zinazochanganya mafunzo yenye malipo ya kazini na masomo rasmi yanayotolewa na Shirika la Mafunzo Lililosajiliwa. Baada ya kukamilisha uanafunzi au mafunzo kazini mtu atakuwa na ujuzi wa vitendo na sifa inayotambulika kitaifa.

Taarifa na msaada unapatikana kwenye tovuti ya ofisi ya uanafunzi ([Apprenticeship Office](#))<sup>1</sup> na tovuti ya Msaada ya Uanafunzi ([Apprenticeship Support](#))<sup>2</sup>.

### Nini maana ya uanafunzi kazini?

Wanafunzi wa uanafunzi kazini hufunzwa ufundi stadi na kuwa mfanyakazi aliyehitimu mwenye sifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VET) inayotambulika kitaifa. Uanafunzi ni mpangilio wa mafunzo uliopangwa wa kawaida wa miaka 3.5 au minne. Mafunzo hayo yanachanganya uzoefu wa kiutendaji kazini na mafunzo ya ziada ya nje ya kazi na Shirika Lililosajiliwa la Mafunzo.

### Nini maana ya mafunzo kazini?

Wanafunzi wa mafunzo hupata ujuzi katika eneo la ufundi stadi na kupata sifa ya VET inayotambulika kitaifa wanapohitimu. Mafunzo hayo yanatoa uelewa wa tasnia na fursa za ajira zinazopatikana. Mafunzo ni makubaliano ya mafunzo kati ya mwanafunzi na mwajiri wake husika ambapo mwajiri anakubali kumfunza mwanafunzi katika tasnia maalum, na mwanafunzi anakubali kufanya kazi na kujifunza. Mafunzo kawaida huchukua kati ya miezi tisa hadi 48, kulingana na eneo la tasnia na kiwango cha cheti kinachofanywa.

### Uanafunzi na mafunzo kazini katika mazingira ya shuleni

Uanafunzi na mafunzo ya msingi shuleni ni mipango ya mafunzo ya ajira yenye malipo kati ya mwanafunzi wa shule wa kutwa na mwajiri.

Uanafunzi na mafunzo kazini katika mazingira ya shuleni huwaruhusu vijana kuchanganya masomo yao ya shule ya juu na ajira ya muda yenye malipo na mafunzo ya nje ya kazi na Shirika Lililosajiliwa la Mafunzo. Wanafunzi hukuza ustadi wa kuajiriwa kupitia uzoefu wa tasnia ndani ya mahali pa kazi halisi na kusoma sifa inayotambuliwa kitaifa. Uanafunzi au mafunzo ya msingi shuleni huwa sehemu ya mpango wa elimu mpana wa mwanafunzi.

### Uanafunzi na mafunzo kazini katika mazingira ya shuleni ni kwa ajili ya nani?

Chaguo hili ni la wanafunzi ambao wangependa kufuata njia ya taaluma katika ujuzi au taaluma mahususi na pia wanataka kukamilisha masomo yao ya elimu ya juu

---

<sup>1</sup> <https://www.dtwd.wa.gov.au/apprenticeship-office>

<sup>2</sup> <https://www.apprenticeshipsupport.com.au/Apprentices/What-is-an-apprenticeship>

## **Je, shule inahitaji kuidhinisha mpango wa mafunzo wa mwanafunzi?**

Fursa za uanafunzi na mafunzo kazini katika mazingira ya shuleni lazima ziidhinishwe na shule kama sehemu ya mpango wa jumla wa shule wa mwanafunzi.

## **Pata maelezo zaidi kuhusu uanafunzi na mafunzo kazini katika mazingira ya shuleni**

Waratibu wa VET wa shule wataweza kutoa taarifa na ushauri kuhusu uanafunzi na mafunzo kazini katika mazingira ya shuleni. Taarifa zaidi inaweza kupatikana kwenye tovuti ya Idara ya Mafunzo na Maendeleo kazini ([Department of Training and Workforce Development](https://www.dtwd.wa.gov.au/apprenticeship-office/apprenticeships-traineeships-for-secondary-school-students)<sup>3</sup>) na katika tovuti ya Kazi na Ujuzi WA ([Jobs and Skills WA](https://www.jobsandskills.wa.gov.au/training/schools-and-school-students)<sup>4</sup>).

---

<sup>3</sup> <https://www.dtwd.wa.gov.au/apprenticeship-office/apprenticeships-traineeships-for-secondary-school-students>

<sup>4</sup> <https://www.jobsandskills.wa.gov.au/training/schools-and-school-students>